KISWAHILI سواحلي

# Saum ni Aina mbili

**Sunnah:** ni saum Zisizokuwa za wajib.

**Wajib:** kama vile ramadhan na saum ya kafara na saum ya kuapa.

**Maana ya saum**


Ni kuabudu Allah kwa kujizuia kukula na kukunywa na kukaa mbali na vitu zote zinazovunja saum kutoka fajr mpaka jua Itue.

## Saum iko na nguzo mbili

### 1 Nia

| Nia ya saum ya sunnah | Nia ya saum ya wajib |
|---|---|
| Inasihi kuweka nia wakati wowote wa mchana maadamu haja fanya vitu zinazovunja saum Lakini thawabu inaanza wakati wa kuweka nia. | Katika saum ya wajib ni lazima kuweka nia usiku yaani Kabla ya fajr. Na inatosheleza kuweka nia wakati mwezi wa ramadhan imeingia. Na mahala pa kuweka Nia ni moyo na kuisema na mdomo ni bid'a. |

### 2 kukaa mbali na vitu zinazovunja saum



**Vitu zilizoruhusiwa kwa aliyefunga.**

- Kuonja chakula kwa haja.
- Kumeza mate.
- Kufanya ghusl.
- Kutumia Mswaki.
- Kupaka manukato.
- Kuoga.

**Vitu zinazovunja saum**

1-kukula na kukunywa kwa kusudi, atakayesahau saum yake ni sahihi 2-kufanya kitendo cha ndoa. Kama ni Mchana katika saum ya wajib anafaa alete kafara.
3-Kutoa mani. 4-Zilizokuwa mfano wa vyakula na vinywaji kama vile sindano iliyokuwa na chakula. 5-Kutoa damu kwa njia ya hijama.
6-Kujilazimisha kutapika
7. Kutokwa na damu ya hedhi au nifaas.

## Sharti zinazofanya saum iwe wajib

1. Kuwa muislamu
2. Kuwa na akili timamu
3. Kufika umri wa kubaleghe, ama asiyefika umri wa kubaleghe anahimizwa kufunga na anaamrishwa na wali wake.
4. Asiyekuwa msafiri. Saum si lazima kwa msafiri. Ni vizuri zaidi afunge saum kama hata pata uzito kulingana na kitendo ya mtume na kwa sababu ni rahisi kuliko kujiekea deni ya ramadhan na pia kutafuta fadla ya mwezi wa ramadhan.
5. Kukuwa na siha.
6. Kutokuwa na hedhi au nifaas

**Vitu ambazo ni haramu kufanya kwa aliyefunga:**

1. Kumeza kohozi lakini haivunji saum
2. Kupiga busu kwa asiyeweza kujimudu.
3. Kufanya uovu ambaye ni haramu.
4. Ujinga.
5. Kufunga saum mfululizo siku mbili bila ya kufuturu.

**Vitu zinazochukiza kufanya kwa aliyefunga**

1. Kuzidisha kwa kuweka maji kwa mdomo na mapua wakati wa kutawadha.
2. Kuonja chakula bila haja.